

- 1. Tuna amini kwamba Biblia inayo ufufuo wa Roho Mtakatifu, neno pekee la Mungu lililo la kweli na lenye mamlaka kwa mambo yote ya kiroho na kimwili.**  
*Kumbukumbu la torati 4:2, Zaburi 19:7-9, Mithali 30:56, Ikor 2:13, Wakalatia 1:8-9,  
II Tim 3:15-17, II Pet 1:20-21, Ufunuo 22:18-19.*
- 2. Tunaamini Mungu moja aishiye milele, Mungu wa utatu, Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu.**  
*Mwanzo 1:1-3, Isaiya 44:6-8; Matayo 28:19-20; Marko 12:29; Yohana 1:4;  
Matendo ya mitume 5:3-4; II Korintho 13:14.*
- 3. Tuna amini katika Mungu Baba asiye na mwisho, nafsi moja mtakatifu aliyejaa hekima nguvu na upendo. Tuna amini kuwa yeye hujishughulisha kwa neema katika mambo yetu yote na kwamba husikia na kujibu maombi yetu na kutusamehe dhambi na kuwaokoa na mauti wote wamjiao yeye kwa njia ya Yesu Kristo.**  
*Mwanzo 21:33, Isaiya 40:28, Kutoka 33:14, Yohana 4:24, Ufunuo 4:8, Warumi 11:33-34,  
Yeremia 32:17, Waefeso 1:19-20, Yeremia 31:3, Warumi 5:8, IISamweli 24:14, IYohana 5:14-15.*
- 4. Tuna amini katika Mungu mwana, Yesu Kristo aliye Mwokozi mwana wa pekee wa Mungu Baba kwa uungu wake katika kusaliwa kwake, na Bikira katika maisha yake yasiyo na dhambi(Mtakatifu) katika miujiza yake, katika kifo chake cha upatanishi ulijotufia sisi kwa kumwaga damu yake katika ufufuo wa mwili wake na kuketishwa kwake kw mkono wa kuume wa Baba. Katika kudumu akiwaombea watu wake na katika kurudi kwake mara ya pili kwa nguvu na utukufu.**  
*Yohana 1:1-2, 14,18;3:16; Luka 1:34-35;24:27, Waebrania 14:15; Warumi 3:23-26;8:34;  
Marko 8:38; Matayo24:30; I Wakorintho 15:3-4.*
- 5. Tuna amini katika Mungu Roho Mtakatifu, msaidizi na mfariji katika uongozi wake wa kila siku na ufunuo wa kweli katika udhihirisho wa dhambi, haki na hukumu na katika uwepo wake ndani yetu katika wokovu kuwawezesha wanao amini kuishi maisha matakatifu ya Mungu.**  
*Yohana3:5-8; 14:16-17; 16:13-14, Matendo ya Mitume 1:8; I Wakorintho 12:13; Waefeso 4:30-32; 5:8;*
- 6. Tuna amini kwamba kila mwanadamu amezaliwa na asili ya dhambi kwa hivyo anahitaji kuokolewa kufanywa upya kwa njia ya Roho Mtakatifu ni ya muhimu sana kwa ajili ya wokovu. Kwa njia ya kutubu dhambi na kupokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yetu.**  
*Yohana 3:5-8; 5:24; Waefeso 1:6-7; 2:8-9; Tito3:5; I Petero 1:23; Matendo ya Mitume2:21;*
- 7. Tuna amini katika ufufuo wa walio okolewa na wenye dhambi na walio okoka katika ufufuo wa uzima wa milele na wenye dhambi katika ufufuo na hukumu ya milele.**  
*Luka 16:19-26;II Wakorintho 5:8; Wafilipi 1:23; II Wathesalonike 1:7-9; Ufunuo 20:11-15.*
- 8. Tuna amini katika umoja wa kiroho kwa wale wote wanao amini Bwana wetu Yesu Kristo.**  
*Matayo 28:19; Matendo ya Mitume 2:42-47; Warumi 15:5-6; I Wakorintho 11:23-26; 12:13.*